Wataalamu wa Vikwazo
Walimu wa Utiifu

Shirika la Kimataifa la Uhodari wa
Uwezo & Utiifu, LLC

26 Juni, 2019

NGUZO YA 1 YA MJENGO SALAMA:

MAMLAKA ZA USHURU KWA MAMLAKA ZA USHURU

1. Utangulizi

Mnamo Aprili 2019, Mamlaka ya Ukusanyaji Mapato ya Kenya (KRA) iliripoti kuwa kupitia ushirikiano na Polisi wa Kimataifa (Interpol), iliweza kuyapata tena magari kwenye poti ya Mombasa . Ripoti pia ilisema kuwa bidhaa zizo hizo zitarudishwa Uingereza (Kule zilipotoka). Mnamo Mei, Shirika la Utangazaji la Briteni (BBC) liliripoti ufutaji kazi wa Naibu wa Rais wa Gabon, pamoja na waziri wa misitu, baada ya “kontena 300 za kuni kupotea” kwenye poti nchini Gaboni, iliyoripotiwa kuwa inaelekea nchini Uchina. Walifutwa na rais, Ali Bongo.

Mifano hii miwili ni miongoni mwa hali nyingi za uvukaji mipaka ambazo zinaendelea kuripotiwa na nchi wanachama za Shirika la Ushuru Ulimwenguni (WCO). Kinadharia, kwa usaidizi wa WCO, kupambana na mitandao/mifumo ya uhalifu ya kienyeji na kimataifa ya kuvuka mipaka, kama ile iliyorejelewa hapo juu, hakujawahi kuwa rahisi zaidi.

Lakini uingiliaji kati wa wanasiasa na upungufu wa uwezo bado ni changamoto madhubuti kwa nchi wanachama za WCO ambazo hazijaendelea. Maeneo ya vita na nchi na maeneo mengine hafifu kama vile Msumbiji Kaskazini, Somalia, Mikoa ya Mashariki ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), nchi nzima ya Jamhuri ya Afrika ya Kati, miongoni mwa maeneo mengine, yamethibitisha kuwa ni maeneo ambayo ni ngumu sana kufaulu kuingilia kati dhidi ya uhalifu na usafirishaji haramu unaovuka mipaka.

Kuibuka kwa SALAMA

Ili kushughulikia mashinikizo haya na mashinikizo mengi mengine ya mipaka ulimwenguni, Baraza la WCO liliidhinisha Mpangilio wa Viwango vya Kulinda na Kurahisisha Biashara ya Kimataifa mnamo Juni 2005 – ambayo inajulikana vizuri zaidi kama Mpangilio wa SALAMA. Inanuiwa kutoa mikakati ya kuzuia ugaidi kimataifa, kukusanya mapato kwa usalama, kukuza urahisishaji wa biashara ulimwenguni. Muda unapoendelea kupita, Mpangilio SALAMA umeibuka kama mwitiko wa pamoja wa jamii ya Mamalaka za Ushuru ulimwenguni wa kuitikia vitisho kwenye usalama wa kufikisha bidhaa, na pia kwa kiwango sawia, unasaidia urahisishaji wa bishara salama na halali.

Tangu hapo, nguzo tatu za SALAMA zimetambuliwa kama viendeshaji vya malengo yake. Mamlaka za ushuru, kwa kushirikiana na serikali mtawalia, zimepewa jukumu la kuhakikishakuwa Mpangilio SALAMA unafanya kazi vizuri. Nguzo Tatu ni: i) Mamlaka za

Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru, ii) Mamlaka za Ushuru kwa Sekta Binafsi na iii) Mamlaka za Ushuru kwa Biashara.

Nguzo ya Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru, ambayo inazungumziwa kwenye kidokezo hiki, intoa mwito wa ushirikiano miongoni mwa Mamlaka za Ushuru. Ushirikiano wa karibu wa Mamlaka za Ushuru ni muhimu kwenye udhibiti wa mipaka wenye ufanisi na ili kufuatilia bidhaa haramu, zikiwemo nyenzo ziliwekewa marufuku na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Kidokezo hiki kinajaribu kuangazia uhusiano (Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Uhuru – Nguzi ya I ya Mpangilio SALAMA), changamoto sawia zinazokumba mamlaka za ushuru na kinajaribu kupendekeza nyanja ambapo sera zinaweza kuboereshwa.

Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru

Unaozidi kuongezeka, mwelekeo wa jumuiya ya kimataifa wa kusambaza vidhibiti vya biashara, marufuku na vikwazo vya kimataifa unalihitaji Shirika la Ushuru lisiangazie tu ukusanyaji wa mapato na urahisishaji wa biashara, bali pia likuze usfirishaji salama wa bidhaa halali na lilinde mipito ya bidhaa ulimwenguni. Ili kutimiza kazi hizi mbili, WCO ilibuni Mpangilio SALAMA wa Viwango kama zana ya kimsingi ya nchi wanachama.

Mojawapo kati ya malengo muhimu ya mpangilio SALAMA ni kuimarisha ushirikiano kuwili na anuwai baina ya Mamlaka za Ushuru ili kuboresha uwezo wao wa kugundua na kuonya kwa muda halisi mizigo yenye hatari kubwa kuwa yanakuka vikwazo. Mizigo yenye hatari kubwa inajumuisha nyenzo zilizowekewa marufuku na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, hasa mizigo yenye mizigo inayoweza kutumiwa kwenye usambazaji wa silaha inayoelekea au inayotoka kwenye Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Korea (DPKR). Mifano ya ukiukaji wa azimio la vikwazo vya Umoja wa Mataifa imeripotiwa na Jopo la Wataalamu linaloangazia Korea Kaskazini; wamedokeza shughuli zilizopigwa marufuku zinazofanywa kwa ushirikiano na raia wa Korea Kaskazini nchini Uganda, Tanzania, Namibia, Angola, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, na Msumbiji.

Kipimo cha kupima kama matakwa ya Nguzo SALAMA ya I (Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru) na utekelezaji wake sahihi utasababisha ufuatilizi na ugunduzi wenye ufanisi zaidi wa nyenzo zisizoruhusiwa bado mpaka sasa hakijabainisha ukweli. Katika kutathmini utekelezaji wa nguzo Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka Ushuru, matokeo mawili muhimu yanafaa kupewa kipaumbele:

1. Ni lazima mipango ya mamlaka za ushuru ikuze usafirishaji huria wa bidhaa ili kudumisha usalama wa upitishaji bidhaa kimataifa.

2. Mpangilio unaokubalika kote unaowezesha ubadilishanaji huria na wa kisheria wa upelelezi na maelezo muhimu kwenye ushirikiano baina ya nchi kadhaa wa Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru

Kubadilisha mielekeo ya mizigo

Hata hivyo, ni lazima matakwa haya mawili yazingatie uhalisia wa Mamlaka za Ushuru za leo za mizigo makubwa inayozidi kuongezeka inayopita kwenye vituo anuwai vya kuvuka mipaka. Kimahususi, vituo vikuu vya kuingia nchini kwa bahari vimeonyesha ukuaji uioukuwa haukutarajiwa. Tunapolinganisha mwaka kwa mwaka, poti za Mombasa zimeripoti ukuaji wa 14.3% wa mizigo iliyoshughulikiwa mnamo Juni 2019. Data ya 2018 hadi 2019 inalingana na ruwaza za muda mrefu za ukuaji. Mnamo 2005, poti iliingiza 436,671 Vizio Sawia Ishirini – TEU-(Kontena); mwaka mmoja baadaye, kiasi cha mizigo kilizidi TEU milioni 1.2.

Mielekeo sawia ya ukuaji inaripotiwa huko Dar es Salaam, ambayo ilishughulikia TEU 287,948 mnamo 2005. Kiasi cha upitishaji kontena kiliongezeka hadi TEU 590,763 kwenye mwaka 2012/13 na zaidi ya 800,000 kwenye mwaka wa 2018.

Bila kurekebisha itifaki za ukaguzi na uingizaji, kulazimu Mamlaka za Ushuru kote ulimwenguni ziache usindikaji pweke wa jadi wa mizigo na zitumie taratibu zenye uwiano kimataifa hakutosaidia kufikia malengo makuu ya kurahisisha biashara ya kimataifa na kudumisha usalama wa upitishaji bidhaa.

a) Ukaguzi Mahiri wa Maelezo wa Elektroniki

Ni lazima mamlaka za ushuru ziwe na uwezo wa kukagua na kutathmini mizigo na nyenzo za usafiri kabla ziwasili kwenye kituo mtawalia cha kuingia/kutoka nchini. Mbinu kama hizi zinazozingatia mbeleni za Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru zinasababisha upitishaji bidhaa kwa upesi zaidi na kugundua kwa usahihi zaidi kontena ambazo huenda zinakiuka vikwazo.

Chini ya Nguzo SALAMA ya 1, Uhusiano wa Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru huwa unaungwa mkono na mfumo wa Ukaguzi Mahiri wa Maelezo wa Elektroniki unaosaidia kutambua nyenzo za usafiri (mbinu ya usafiri) na mizigo ambayo huenda inakiuka vikwazo. Mchanganyiko wa mifumo mahiri ya arifa na ukaguzi otomatiki na vifaa vya kulenga unawezesha Mamlaka za Ushuru zidhibiti hatari za mizigo inayoingia kwa kutambua usafirishaji wenye hatari kubwa huku chombo cha usafiri bdo kiko kwenye maji ya kimataifa. Kwa ajili ya arifa za mapema, matayarisho yanaweza kufanywa, ikiwa kuwa na wakaguzi mahiri wa Mamlaka za Ushuru au timu za uchunguzi kwenye egesho waka chomo husika kinapowasili. Kuchukua hatua, kwa muktadha huu, pia kunajumuisha kushiriki hatari zilizotambuliwa na mamlaka zingine husika za ushuru huko ng'ambo na ndani nchini kwenye mamlaka husika, kama vile mamlaka za kudhibiti biashara na watekelezaji sheria wengine.

Licha ya mbinu pweke yenye kinga ya shughuli za Mamlaka za Ushuru kutamatishwa kwenye nadharia iliyobuniwa kwenye Nguzo SALAMA ya 1, ada ya shughuli za Mamlaka za Ushuru barani Afrika inaendelea kushinikizwa na vizuizi vikali vya uwezo. Uboreshaji muhimu ni

kurahisisha ubadilishanaji wa maelezo kwa muda halisi miongoni mwa mamlaka za ushuru kwenye mataifa barani Afrika utakuwa uendelezaji wa teknolojia ya ukaguzi. Inafaa kujumuisha, bila kuwekewa kikomo kwa, mashini kubwa za eskirei na gamarei na vifaa vya kugundua mnururisho. Lakini, hii ni sehemu moja tu ya kusombeza taratibu za Mamlaka za Ushuru. Sehemu ya pili inahusu mbinu ya mawasiliano ambayo itatumiwa kwa ubadilshanaji wa maelezo, upelelezi, na ripoti kwa muda halisi ili kuzisambaza kwa maafisa husika na mamlaka za ushuru ambayo itaruhusu kuingilia kati kwa upesi inapohitajika.

Kwa mfano, ikiwa afisa wa mamlaka ya ushuru mwenye makao yake makuu nchini Kenya anagundua uwezekano wa hatari kwenye ukaguzi wa kawaida wa mizigo ya uuzaji nje, maelezo hayo yanafaa kusafirishwa papo hapo kwa shirika mwenza la Mamlaka za Ushuru kwenye nchi ambapo mizigo hiyo inaelekea. Maafisa wa mamlaka za ushuru wanafaa kushirikiana na kuendelea kufanya kazi na washiriki wao kimataifa na kuwezesha njia na mbinu za si tu kushiriki maelezo, bali pia kupanga mipango ya matendo yenye lengo la kudumisha usalama wa upitishaji bidhaa.

Hata kama, kinadharia, matumizi ya teknolojia mahiri zaidi yatakubaliwa na nchi zinazostawi na Mamlaka zao za Ushuru, lakini bado kuna maswali yasiyokuwa na majibu kuhusu jinsi yatakavyoweza kuipata na nani atafunza wafanyakazi wao jinsi ya kuitumia teknolojia hiyo vizuri. Kivingine, ari kubwa sana ya kisiasa inahitajika ili mawakala ya Ushuru yaweze kufahamishwa kikamilifu kwenye maeneo yote ulimwenguni.

Alama ya Biashara kwenye Afrika Mashariki (TMEA), ni wakala inayofanya shughuli zake kwenye eneo la Afrika Mashariki, imekuwa kwenye safu ya mbele ya kusaidia mawakala ya kutekeleza sheria ya serikali za Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikiwemo mamlaka za ushuru, ili kushughulikia vizuri zaidi changamoto za teknolojia na miundombinu. Kutokana na ripoti yake, TMEA inasema kuwa takriban 38% ya bajeti yake inalenga nyanja ya "Mazingira ya Biashara Yaliyokuzwa;" kiasi kingi cha bajeti kimeteuliwa ili kuboresha uratibu wa kieneo na kimataifa kupitia kukuza uwezo wa matawi, taasisi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, na wizara kwenye kila Nchi Shiriki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Athari yake itajitokeza mbeleni lakini tayari inaonekana kwani jitihada na shughuli kadhaa za pamoja za mamlaka za ushuru za eneo ambazo wakala hii imekuwa inazitekeleza kwenye eneo hili. Mojawapo kati ya mafanikio muhimu ya TMEA ni uundaji wa Jitihada za Mipaka ya Pamoja ambazo zimewezesha, kwa mfano, Mamlaka za Ushuru za Uganda na Kenya zifanye kazi pamoja kwenye mpaka wa Malaba. Jitihada sawia inatumiwa kwenye mpaka wa pamoja wa Namanga (Kenya na Tanzania). Kwenye mivuko hii ya mipaka, maafisa wa mamlaka za ushuru wanafanya kazi pamoja, wanabadilishana maelezo, na wanatekeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi – kama vile Nguzo SALAMA ya 1 ya Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru ilivyonuia.

Wahusika wengine, kama vile Wakala ya Ushirikiano Kimataifa ya Japani (JICA), pia wamekuwa wanarahisisha ushirikiano wa Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru kupitia jitihada za pamoja za kujenga uwezo kama vile Udhibiti wa Hatari kwa maafisa wa Ushuru kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Jitihada na shughuli hizi za pamoja zinazofanywa na

TMEA na JICA zimechangia kwenye kuboresha uhusiano wa kikazi miongoni mwa wasimamizi wa mamlaka za ushuru kwa maafisa husika wa mamlaka za ushuru na shirika lao kwenye eneo.

Nguzo ya Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru ya Mpangilio SALAMA inalenga uboreshaji zaidi wa viwango kwa mamlaka zote za ushuru:

- Usimamizi Uliowianishwa wa Mfululizo wa Ufikishaji;
- Mamlaka ya Ukaguzi wa Mizigo;
- Teknolojia ya Kisasa kwenye Vifaa vya Ukaguzi;
- Mifumo ya Kudhibiti Hatari;
- Mzigo au Kontena yenye Hatari Kubwa;
- Maelezo ya Mapema ya Elektroniki;
- Kulenga na Mawasilianon;
- Vipimo vya Utekelezaji;
- Tathmini za Usalama;
- Uadilifu wa Waajiriwa
- Ukaguzi wa Usalama wa Bidhaa Zinazotoka.

Kwa hivyo - tatizo ni nini?

Kumekuwa na ripoti anuwai za usafirishaji wa bidhaa haramu unaofanywa na magenge ya kihalifu kwenye poti na bandari nyingi barani Afrika. Mifumo ya ndani ya upelelezi ya sekta ya usafiri baharini imejaa ripoti za magenge ya kihalifu kuingiza mizigo isiyoruhusiwa kwenye bandari ndogo za kibiashara, ambazo mara nyingi hazisimamiwi daima na maafisa wa Mamlaka za Ushuru, kwenye pwani ya mashariki barani Afrika. Vituo vilivyoamilifu kisehemu vinatoka Kismayu nchini Somalia hadi Angoche nchini Msumbiji. Hata poti kubwa zinahusishwa kwenye tendo hili haramu kisheria. Mitandao ya uhalifu pia imejiingiza na kutumia vituo vya mipaka ya ardhi vinavyotumika kiasi na, kwenye baadhi ya maeneo, hata pia viwanja vya ndege vya pili na tatu. Baadhi ya mitandao ya kihalifu mara nyingine huwa ina athari kwa viongozi wa siasa na siasa za baadhi ya nchi wanachama. Ripoti za magenge ya dawa za kulevya kukampeni ili kupata nyadhifa za kisiasa moja kwa moja au kivingine zimeripotiwa. Kwa kukusanya nguvu nyingi hivi, magenge ya uhalifu yanaweza kupata dara za juu za ulinzi wa kisiasa na uwezo kufanya karibu chochote watakacho.

Magenge ya kimataifa yameripotiwa kuwa yanafanya shughuli kwenye vituo vya kuingia barani Afrika na kwengine. Ripoti kutoka timu ya ufuatilizi wa Usalama ya Umoja wa Mataifa iliashiria kuwa, kwenye vurugu la Somalia, vikundi vya wanamgambo vimeanza kunufaika kutokana na dawa za kulevya zinazoletwa nchini Kenya. Poti kuu kwenye Somalia kusini iko Kismayo, mji unaodhibitiwa kikamilifu na al-Shabaab, ambayo inapata bidhaa kupitia poti ya Kismayo na ambayo inatumia mifumo ya kutoza ushuru kwenye poti kama chanzo cha mapato."

Hivi karibuni, rais wa Jamhuri ya Kenya amekuwa kwenye safu ya mbele ya kupigana dhidi ya biashara haramu ya bidhaa bandia. Miongoni mwa watu wanaohusika kwenye biashara hii haramu huwa wanafanya kazi na maafisa wa serikali, wakiwemo wasimamizi wa mamlaka za

ushuru. Hii inaweza kujitokeza kwa mbinu ya kuuza maelezo kwa vikundi vya uhalifu, kurahisisha upitishaji wa bidhaa haramu, na kuzuia uchunguzi. Ni wazi kuwa vitendo hivi hramu huwa vinaathiri vibaya uwezo wa mashirika ya Mamlaka za Ushuru na vinapunguza manufaa yawezekanayo ya ushirikiano wenye ufanisi wa Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru. Tamaduni ya kupuuza uhalifu kwenye eneo inaathiri vibaya uchumi na biashara. Kwa hivyo, ni lazima mielekeo hii ikomeshwe na ufanisi wa watekelezaji sheria, wakiwemo watekelezaji wa Mamlaka za Ushuru, ukuzwe.

1. Uwezo wa Mamlaka za Ushuru

Mafanikio ya utekelezaji wa Nguzo SALAMA ya 1 yanategemea matokeo mawili:

- Ubadilishanaji huria wa maelezo baina ya mamlaka za ushuru;

- Ufikishaji wa utambuzi sawia wa vidhibiti kwenye masharti fulani. Utambuzi sawia hapa unarejelea mipangilio iliyoundwa na mamlaka mtawalia za Ushuru ambayo imekubaliwa kwa malengo ya uhalalishaji na uidhinishaji. Kwa mfano, mamlaka mbili za Ushuru zinaweza kubuni utambuzi sawia kuwa ikiwa bidhaa “zimekaguliwa” na mmoja wao na bidhaa sawia zinaletwa kama mamlaka ya pili ya ushuru. ukaguzi uliofanywa unaheshimiwa na hakuna haja ya kukaguliwa tena mamlaka inayopokea bidhaa hizo. Mipangilio hii inahitajika ili kuangamiza na kupunguza marudio ya juhudi za uhalalishaji na uidhinishaji.

Hivi ni vifaa vinavyohitajika ili kuunda mazingira yanayowezesha utekelezaji sheria wenye ufanisi wa Mamlaka za Ushuru.

Kwa mamlaka nyingi za ushuru za nchi zinazostawi, vifaa kama vichanganuzi vya eksirei ni ghali kununua na gharama za udumishaji zinasababisha gharama za ziada za fedha. Hata hivyo, inafaa kuzingatiwa kuwa mamlaka nyingi za ushuru barani Afrika zimefaidika na nchi zinazofadhili ambazo zimewezesha mamlaka hizo zipte baadhi ya vifaa hivi. Uboreshaji huu umekuza sana kazi ya shughuli za Mamlaka za Ushuru nchini Uganda ambapo, kwa mfano, vichanganuzi vya eksirei vimetumiwa ili kugundua pembe na kakakuona. Vivi hivi, mnamo Februari 2019, Sudani Kusini, kwa kutumia vichanganuzi kutoka Uingereza, iligundua pembe zilizofichwa kwenye kontena zilizokuwa zinaelekea barani Asia.

Kwenye karne ya nyenzo otomatiki, kuna haja ya kuunganisha vichanganuzi na mifumo mikuu ya usindikaji ushuru ya nyingi kati ya nchi hizi. Uwezo wa vichanganuzi hii kuunganisha kazi ya vifaa hivi na mfumo mkuu wa upitishaji wa mamlaka za ushuru unafahamika vizuri. Hata hivyo, si maeneo/vituo vyote vikuu vya mipaka vilivyohamiwa na zana hizi.

2. Ufisadi

Kulingana na shirika la Transparency International, nchi nyingi barani Afrika zina daraja mbaya kuhusiana na fahirisi ya ufisadi. Imeripotiwa kuwa ufisadi huu upenyeza taasisi nyingi za

serikali, zikiwem huduma za Mamlaka za Ushuru. Pasipokuwepo mfumo madhubuti wa kudhibiti hatari (tazama hapo chini), asili halisi na mbinu ya utendakazi ya Mamlaka za Ushuru inawapatia uamuzi mwingi maafisa, kwa mfano, kwenye kuchagua ni mizigo ipi ikaguliwe na ipi ipuuzwe. Utendakazi huu wa uamuzi unaweza kutumiwa vibaya ambayo inaweza kusaidia walanguzi na uhalifu wa kimafia, ambayo inavunja lengo zima la kutekeleza sheria za mamlaka za Ushuru. Sababu nyingi, ikiwemo mazingira taabu ya kufanya kazi, mishahara midogo, au fursa ndogo za kupandishwa cheo, pamoja na uwezekano mkubwa wa kufanya makosa bila kugunduliwa, ni vishawishi vya kupokea hongo au mbinu zingine za ufisadi.

Ili kufaidika kikamilifu na mbinu ya uhusiano wa Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru, ni lazima nchi barani Afrika na nchi zingine kote ulimwenguni zijitolee kupigana na ufisadi, hasa kwenye mawakala ya serikali kama vile mamlaka za ushuru.

3. Ari ya kisiasa

Kwa ajili kuna maslahi mengi yanayopingana, mashinikizo ya bajeti yasiyoisha, na kutengewa fedha kidogo zaidi kwenye bajeti, maingiliano na kisiasa ya maafisa wakuu serikalini yanaweza kuhakikisha kuwa mashirika ya Ushuru yamehamiwa na kutayarishwa ili yatekeleze wazo la Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru. Mahitaji haya ya kisiasa yanaenda kinyume na nchi nyingi kwenye ulimwengu unaostawi, ambapo wanaofanya maamuzi ya kisiasa wanaachiwa mashinikizo ya bajeti ambayo yanaweza kuhimiliwa tu kwa kutumia utatuzi wa muda mfupi wa ukusanyaji mapato wa Mamlaka za Ushuru.

Hata kama maamuzi haya yanaweza kueleweka, huwa yanatupa mbali manufaa ya kudumu na halisi zaidi ya kudumisha usalama wa upitishaji bidhaa kwa muda mrefu. Kubadilisha mawazo ya viongozi wakuu seriklini kutawezesha utekelezaji wenye ufanisi wa Nguzo ya 1 ya Mpangilio SALAMA na upitishaji bidhaa wenye manufaa zaidi.

Kwa mfano, kumekuwa na ripoti kuhusu simtofahamu miongoni mwa mawakala ya mipaka kwenye baadhi ya nchi za Afrika Mashariki. Kwa asili yake, hii haiungi mkono mtandao wa Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru. Usimamizi wa mipaka wenye ufanisi unahitaji serikali ziendelee kufanya kazi kwa kushirikiana kwenye hali ya ‘’mfuatano’. Ili kutimiza lengo hili, ushirikiano ni muhimu.

Lakini si rahisi kushirikiana ikiwa, kwenye kituo cha kawaida cha mipakani, mawakala kadhaa ya taifa yana matakwa ya kulinda, kudhibiti, na kupata mapato bila kuwa na haja ya kushiriki matakwa ya kushirikiana wao kwa wao au kushirikiana na mawakala wenza kwenye upande mwingine wa mpaka. Kushiriki maelezo kwenye pande mbili za mpaka baina ya wahusika walioko kwenye safu ya mbele, kwa mfano baina ya maajenti wa Mamlaka za Ushuru za Kenya na Somalia, ni muhimu ili kuzuia kuenda kinyume na vikwazo, kuzuia usafirishaji haramu, na shughuli zingine za kihalifu. Kwenye mandhari ya mipaka baharini, ukosefu wa kushiriki maelezo ya Mamlaka za Ushuru unasababisha udhaifu mbaya zaidi, kama vile uharamia, au kuwachukua mateka wafanyakazi wa kutoa misaada au usaidizi mwingine wa kibinadamu.

Machaguo ya sera na uhalisi wa sera za kitaifa

Ubadilishanaji huria wa maelezo miongoni mwa mamlaka za Ushuru ndiyo kigezo kikuu cha mtandao wa Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru. Ili kuzidi kurahisisha lengo hili, WCO imebuni na kutumia Ofisi za Kieneo za Uwiano wa Upelelezi (RILO). Mpangilio wa RILO unajumuisha ofisi za kieneo zinazohudumia maeneo wazi na mtawalia ya WCO. Matakwa yake muhimu ni kuratibu mawasiliano, kuhimiza ubadilishanaji wa maelezo miongoni mwa shughuli za Mamlaka ya Ushuru ya taifa, na, kimahususi, kuhakikisha mawasiliano kwa muda mwafaka ya upelelezi muhimu.

Kila nchi mwanachama inatarajiwa kuwa na kituo kikuu kwenye usimamizi wake ambaye atakuwa mwasiliani wa kwanza wa ofisi ya kieneo ya RILO wa kubadilishana maelezo na kuingilia kati ili kuzuia uhamishaji haramu mipakani. Wazo la RILO halifanyi kazi tu kwa msingi wa kuhitaji kujua. Ubdilishanaji huria wa maelezo pia unajumuisha mwingiliano endelevu na mtiririko wa kuvuka mipaka wa maelezo bila kuhitaji “kuyaulizia” maelezo hayo. Mtandao madhubuti unaoungwa mkono wa RILO unaweza kufanyia mengi zaidi ubadilishanaji huria wenye ufanisi wa wa maelezo ambao kwa muda mrefu, utasaidia nguzo ya Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru inayozungumziwa hapa.

Ingawa WCO inahimiza nchi wanachama zikubali itifaki hizi za ushirikiano na inapendekeza uratibu zaidi kwenye ubadilishanaji wa maelezo, matumizi halisi ya itifaki hizi yamekawia. Bila kujali makubaliano saidizi baina ya nchi mbili na nchi kadhaa, nchi barani Afrika hazioni njia ya kuelekea kwenye utekelezaji kamili huku zinashughulikia changamoto, vizubaishi, na mashinikizo mengine ya bajeti. Kuna haja ya kuwa na juhudi za kimakusudi, mara nyingine hata juhudi za kieneo, ili kuleta ushirikiano wa karibu zaidi na ukuzaji wa ushirikiano wa Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru. Hii haitosaidia mamlaka za ushuru zidhibiti mipaka (ikiwemo ukusanyaji mapato) vizuri zaidi, bali pia itasaidia kuufanya ulimwengu uwe salama zaidi.

Kama mfano wa ushirikiano wa Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru, Mamlaka ya Ushuru ya Kenya ilitekeleza mfumo wa kupitisha bidhaa wa Mamlaka ya Ushuru mnamo 2005 unaoitwa Simba. Mbeleni, ilikuzwa kwa moduli inayotoa uwasilishaji wa kudumu na wa mara kwa mara wa maelezo hadi kwa Mamlaka ya Ushuru ya Uganda, ikiwemo kuonya kielektroniki kuhusu mizigo nyeti inayosafirishwa. Kwa mujibu wa mtiririko huu wa maelezo kwa muda halisi, Uganda inaweza kuchukua hatua zinazohitajika mapema pale inapohitajika. Kenya pia ilifaidika kutokana na uwasilishaji wa SImba kwa sababu, wakati data ilipojumuishwa kwa mitiririko yote ya mizigo, baadhi ya mizigo ilipatikana kuwa haikuwasili nchini Uganda; badili yake ilibwagwa nchini Kenya. Hii ilimaanisha kuwa Kenya ingeweza kuidhinisha hatua za utekelezaji sheria zinazohitajika kwa bidhaa ambazo hazijathibitishwa kuwa zimepokewa nchini Uganda. Hatua hizi za utekelezaji sheria zilijumuisha ukusanyaji wa mapato. Kwa malengo ya kukusanya mapato, Simba ilikuwa ushindi pande zote mbili kwa Kenya.

Kwenye Afrika Mashariki, mamlaka zote za ushuru zina mifumo ya mtandaoni ya upitishaji bidhaa. Uganda inaendesha Mfumo Otomatiki wa Data ya Mamlaka ya Ushuru (ASYCUDA);

Kenya ina mfumo wa Simba; Tanzania ina Mfumo Jumuishi wa Mamlaka ya Ushuru ya Tanzania (TANCIS). Ingawa nchi hizi tatu zinafanya shughuli kama eneo moja la mamlaka ya ushuru lenye sheria zilizowianishwa na ushuru wa sawia wa nje, mifumo hii ya upitishaji bidhaa haijaunganishwa, haiwasiliani, na kwa hivyo yanaleta kizuizi kingine kwenye mbinu ya kudhibiti hatari ya Mamlaka za Ushuru. Hii ndiyo changamoto inayozikumba mamlaka hizo za ushuru na labda hatua zinazohitajika zinafaa kuchukuliwa ili kuhakikisha kuwa haya yanashughulikiwa.

Kama sehemu ya mazungumzo haya, WCO imebuni vifaa kadhaa vya IT na kuviweka viweze kutumika na wanachama wake; vikitumiwa kikamilifu, vifaa hivi vinaweza kusaidia sana ili kuboresha ushirikiano wa mamlaka za ushuru kwa mamlaka za ushuru. Vifaa hivi vya IT vinajumuisha:

a) Mtandao wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mamlaka za Ushuru (nCEN). Kifaa hiki kinawapatia wasimamizi wa Mamlaka za Ushuru uwezo wa kukusanya, kuhifadhi, kuchambua, na kusambaza maelezo ya daraja ya taifa yanayohusu, si wao tu, bali pia mawakala mengine ya kutekeleza sheria. nCEN inaipatia Mamlaka ya Ushuru fursa ya kuimarisha upelelezi imara na uwezo wa kuainisha ambao unaweza kuusaidia ushirikiano wa Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru ikiwa utatumiwa.

b) Mfumo wa Kulenga Mzigo (CTS). Kifaa hiki kimeundwa kimsingi ili kuwezesha Mamlaka za Ushuru zinase data ya orodha ya mizigo ya hewani na baharani kwenye “umbizo la elektroniki na kuchambua data iliyokusanywa ili kutambua usafirishaji wenye hatari kubwa ya kukiuka vikwazo wa uingizaji nchini, uuzaji nje, na usafirishaji wa kimpito kwenye mfululizo kamili wa vitisho kwa Mamlaka za Ushuru,” ikiwemo ukiukaji wa nyenzo zilizowekewa marufuku ya Umoja wa Mataifa.

Vifaa hivi binahitaji kuidhinishwa na kutekelezwa kikamilifu na nchi wanachama za WCO ili ziweze kupata manufa kamili ya ushirikiano wa Mamlaka za Ushuru kwa Mamlaka za Ushuru.

Kuhusu Thomas Bifwoli

	Thomas Bifwoli amefanya kazi na Mamlaka ya Ukusanyaji wa Mapato Nchini Kenya (KRA); na aliidhinishwa awe Mkubwa wa Ofisi wa Ofisi ya Ushirikiano ya Upelelezi wa Kieneo ya Shirika la Ushuru Ulimwenguni ambayo ni ya Afrika Mashariki na Kusini (WCO RILO ESA). Alifanya kazi kama mratibu wa kundi la wataalamu wa ufuatilizi wa

	vikwazo vya Umoja wa Mataifa.